# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Awali ya yote, napenda kuelekeza shukurani zangu kwa Mtukufu wa Ulimwengu na muumbaji wa Viumbe vyote mbinguni na ardhini kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kupitia na kujadili utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yaliyowasilishwa katika Baraza hili tukufu katika Mkutano wa Baraza wa mwezi wa Febuari 2022, mwaka huu. Aidha, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa juhudi mnazochukua za kuliongoza Baraza hili kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu.

**Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kuthamini juhudi anazochukua Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi za kutekeleza ipasavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza ahadi zake ambazo aliwaahidi wananchi wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 sambamba na kuendelea kutunza hali ya Amani, Utulivu pamoja na kuimarisha hali ya siasa kwa kuwaunganisha Wazanzibar kuwa kitu kimoja.

**Mheshimiwa Spika,** Nitakuwa sijatenda haki, ikiwa nitaacha kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalluh kwa umahiri wake mkubwa wa kuyasimamia vyema majukumu ya Wizara zote za Serikali ambapo Zanzibar na wananchi wetu wanamatumaini makubwa ya kunufaika na utekelezaji wa Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia msingi wa Kanuni ya 109 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020, nimesimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kusema machache kati ya mengi juu ya mambo muhimu yanayohusu Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC ya mwaka 2019/2020 iliyowasilishwa hivi punde na Waziri wa Fedha na Mipango mbele ya Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,** Nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, na Mipango; Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, Naibu Waziri; Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir (Mrembo), Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hi kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Kwa kweli tunawashukuru sana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa napenda kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya PAC kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ushirikiano wa hali ya juu. Mheshimiwa Spika, Wajumbe hawa wamekuwa wakishiriki mijadala ya vikao vya Kamati kwa umakini mkubwa na kutumia vyema Elimu, Taaluma, Uzoefu na Vipaji vyao katika kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za Hesabu pamoja na taarifa nyengine zinazoletwa katika Kamati, na kutoa ushauri ambao umeifanya kazi ya Kamati hii kuwa na ufanisi mkubwa. Nawashukuru pia Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati.

**Mheshimwa Spika**, kwa ruhusa yako, naomba sasa niwatambue Wajumbe na Makatibu hao wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Juma Ali Khatib - Mwenyekiti;
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe;
4. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe;
5. Mhe. Sulubu Kidongo Amour - Mjumbe;
6. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe;
7. Ndg. Maryam Haji Ali - Katibu; na
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa katika Mkutano wa Febuari 2022, Kamati ya PAC iliwasilisha katika Baraza lako Tukufu Maoni, Ushauri na Mapendekezo lukuki yaliyotokana na ufuatiliaji wa Ripoti Nne za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizohusiana na:-

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020;
2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018;
3. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020; na
4. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kiujumla, Kamati yetu imebaini kwamba baadhi ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo iliyoyawasilisha kwa Wizara husika yametekelezwa kwa asilimia mia moja (100%), mengine hayajatekelezwa kikamilifu na mengine yanahitaji muda katika kukamilisha utekelezaji wake. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kubaini kwamba yametekelezwa kama yalivyoelezwa na Watendaji wa Wizara kupitia majibu waliyoyawasilisha kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaupongeza Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kwa huduma za ulinzi inazotoa kwa Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuna madeni ambayo Wakala huo unazidai Taasisi mbali mbali. Kamati yetu inaendelea kuisisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuzikata fedha moja kwa moja Taasisi zilizopatiwa huduma na Wakala huo kutoka katika fedha zao za matumizi mengineyo na kuziingiza katika hesabu (account) ya Wakala wa Ulinzi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo mwanzo mzuri wa wa uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato vilivyofanywa na Jeshi la Kujenga Uchumi kwa kuamua kutenga jumla ya shilingi bilioni moja (1,000,000,000) katika mwaka wa 2022/2023 kwa ajili ya kuanzisha Mradi wa kilimo cha Umwagiliaji maji Unguja na Pemba. Hata hivyo, Kamati ya PAC inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inaliingizia Jeshi hilo fedha hizo kwa wakati ili Mradi walioupanga uweze kutekelezeka na kuleta tija kwa nchi na wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu haikuridhishwa na utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati yetu kwa kushindwa kulipatia ufumbuzi suala la kuwepo kwa maegesho ya gesi katika eneo la Welezo. Hata hivyo, Kamati yetu inaendelea kusisitiza kwamba Taasisi za Serikali ziendelee kulifuatilia kwa karibu suala hili ili ziweze kulipatia ufumbuzi na kuepusha majanga yasiyokuwa ya lazima kutokea kwa watu wanaokwenda eneo hilo kwa ajili ya kujifurahisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaendelea kuipongeza Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kufuatilia madeni wanayowadai watumishi waliowapatia mafunzo kutoka shilingi milioni 32,962,000 hadi kufikia shilingi milioni 7,300,000. Hiyo ni hatua mzuri ya kuigwa na Taasisi nyengine ambazo zinadai madeni kutokana na huduma wanazozitoa. Hata hivyo, Kamati ya PAC inaendelea kushauri kwamba Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ihakikishe inachukua juhudi za makusudi zitakazowezesha deni hilo linalipwa lote na kasoro kama hizo hazijitokezi tena katika ukaguzi utaofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imeridhika na utekelezaji wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mapendekezo yatakayowezesha kuwa na mfumo mmoja wa uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka wa “Accrual” yatakayopelekwa katika Kamati ya Wataalamu ya Makatibu Wakuu kwa kujadiliwa na kufanyiwa marekebisho. Hata hivyo, Kamati yetu inaendelea kuushauri Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuchukua

juhudi za makusudi kuhakikisha inakamilisha kwa haraka hatua zilizobakia kwani kutofautiana kwa mifumo kunasababisha utofauti mkubwa wa ufungaji wa hesabu na kutoa mwanya kwa wabadhirifu kuitumia vibaya mifumo hiyo na kuweza kujinufaisha wao na familia zao badala ya kunufaisha umma kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ya PAC **imesikitishwa na kutofurahishwa** na kitendo cha Wizara ya Afya kwa upande wa Unguja cha kutoipatia ushirikiano Kamati yetu ilipofika Ofisini kwao kufuatilia hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako inafanya kazi kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu ambazo tumezipitisha wenyewe humu Barazani, ambapo Kamati za Kifedha zimepewa jukumu la kufuatilia hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa nia njema ya kupima usahihi na kuweka usawa pale ambapo Mdhibiti ameteleza. Kwa mshangao, baadhi ya Taasisi za Serikali hubeza jukumu hilo na kuamua kushindwa kutoa ushirikiano ili Kamati zako zisiweze kubaini ukweli uliopo na kushauri ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ina kila sababu kueleza kwa uwazi na bila ya kumung'unya maneno kwamba inaungana na hoja zote zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinazohusiana na Wizara ya Afya kwa upande wa Unguja (zinazopatikana kuanzia ukurasa wa 125 hadi 129 za kitabu cha Ukaguzi wa Fedha za Serikali Kuu) kwani Kamati yetu ilikosa majibu fasaha na vielelezo vitakavyowatoa wao katika tuhuma. Lakushangaza zaidi, kila walipokuwa wakihitaji vielelezo watendaji walikuwa wakitoka ukumbini kwa sababu ya kwenda kuvileta lakini huwa hawarudi tena ukumbini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilishindwa kufanya kazi katika mazingira ya namna hiyo na kuahirisha kikao hicho. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu imegundua kuna watendaji wa Wizara ya Afya kwa upande wa Unguja wanahusika katika ubadhirifu wa rasilimali za umma ama moja kwa moja au vyenginevyo. Hivyo, ni busara kwa vyombo vinavyohusika na uchunguzi na usimamizi wa sheria za nchi kufuatilia hoja moja baada ya nyengine kwa kuwatafuta wote waliohusika na kuwachukulia hatua za kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa utendaji wa namna kama hii, Kamati yako imesikitishwa kwa kusema kwamba kuna uwezekano wa Mdhibiti kugundua mambo makubwa zaidi katika kila ukaguzi anaoufanya na iwapo hakutokuwa na hatua madhubuti zitakazochukuliwa kudhibiti hali hiyo au kusimamia ipasavyo kasoro hizo, ubadhirifu wa rasilimali za umma zitaendelea kutokea na ile ahadi yenye nia njema na maendeleo ya Zanzibar ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwamba ukaguzi wa mwakani usiwe na hoja hata moja, utekelezaji wake unaweza kukosa ufanisi kutokana na uzembe wa watendaji wachache.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) za kutengeneza mfumo wa kutangaza na kuuzia Vitabu na Makamusi ya lugha ya Kiswahili ndani ya Tanzania. Hata hivyo, ni vyema kwa BAKIZA kutanua wigo wa kuitangaza zaidi lugha hiyo katika maeneo mengine ya Afrika Mashariki kwani kufanya hivyo kutaongeza idadi ya watumiaji na kuiimarisha lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako imefuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ambao kwa asilimia kubwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako wanahusika nao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, kuharakisha mchakato wa sheria ya marekebisho ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ambao ndio yataleta hitimisho ya changamoto nyingi ambazo zinaukabili utekelezaji wa Mfuko huo. Sambamba na utungwaji wa Kanuni za sheria hiyo ili kurahisisha utekelezaji mzuri wa shughuli za Mfuko wa Jimbo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imesikitishwa kwa vitendo vya baadhi ya watendaji kutoa siri za vikao vya Kamati vinavyolenga kuelekezana, kukosoana au kupongezana pale ikibainika kuna jambo zuri limetekelezwa. Kufanya hivyo kunaweza kutengeneza uhasama kwa Wajumbe wa Kamati na watu wengine waliopo nje ya Kamati. Kamati ya PAC inasisitiza kwamba masuala yanayozungumzwa ndani ya kumbi za vikao huwa ni sawa na mambo yanayozungumzwa ndani ya Baraza ambapo Wajumbe huwa na kinga kwa mujibu wa Sheria na hayatakiwi kuelezwa ovyo kwa watu wasiohusika kinyume na maamuzi ya Mkutano husika.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Aidha, salamu zangu za pongezi ziwaendee Wajumbe wa Kamati yangu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa kuweza kukamilisha kazi hii muhimu na adhimu kwa Baraza letu.

**Mheshimiwa Spika,**
Sasa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muunge mkono utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kueleza hayo machache, Kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, naunga mkono utekelezaji huu na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………

**Mheshimiwa Juma Ali Khatib,**
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**